

Huduma ya afya nchini Marekani

Système ya soins de santé nchini Marekani ni mgumu na inaweza kuwa vigumu kui elewa wakati unapo fika. Kumbuka kwamba gundi yako ya usaidizi inaweza kukusaidia kujibu maswali yako na kukupa maelezo zaidi.



Kuelewa Huduma ya Afya nchini Marekani

Kupata matunzo nchini Marekani mara nyingi inaomba kuwa na assurance médicale, ambayo itasaidia kulipia gharama ya matunzo. Kuna aina nyingi ya huduma ya afya:

Medicaid : Mpango wa serikali ambao ina towa assurance ya bure ao malipo ndogo kwa watu wa kipato cha chini, ikiwa ni pamoja na wakimbizi wamoja na wageni. Ma shurti ya ku chaguliwa iko tafauti kulingana na jimbo moja na ingine.


Assurance inayotolewa ku kazi yako : Kazi nyingi ina towa assurance ya afya kama faida. Huenda ukalazimika kulipa sehemu ya garama ya assurance kupitia mshahara wako.

Assurance nyingine : Ikiwa hau eneze shurti inayo ombekana ili ku kupata Medicaid au huna Assurance kupitia kazi yako, unaweza kununua assurance ku marché d'assurance. Usaidizi wa kipesa unaweza kupatikana kulingana na mapato yako.

Watoa huduma za afya

Kuna aina mbalimbali za watoa huduma za afya nchini Marekani. Hapa kuna baadhi yao:

Idara za afya ya kiserkali hutoa chanjo ya kupiganisha magonjwa na huduma zingine za kinga, pamoja na uchunguzi na matibabu ya kifua kikuu. Huduma za kinga za afya ni huduma zinazozuia magonjwa kabla hayajatokea. Kwa kawaida kukutana na daktari inahitajika.



Kliniki za jamii **na vituo vya afya** vinatoa huduma za kimsingi za afya na ushauri wa afya ya akili. Wengine pia hutoa huduma ya meno na machunguzo ya macho. Katika miji, baazi ya kliniki hutibu aina maalum za wagonjwa, kama vile wanawake wajawazito au watu wenye Virus vya UKIMWI. Kliniki zinakubali assurance ya kibinafsi na Medicaid (Assurance ya serikali kwa watu wa kipato cha chini), na nyingi hutoza ada kulingana na uwezo wa mgonjwa kulipa.

Madaktari wa kibinafsi ni madaktari wa jumla au wataalam. Madaktari wa kawaida hutoa huduma ya afya ya jumla, ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kila mwaka. Wataalamu hufanya kazi katika eneo ya kipekee ya matunzo. Wataalamu wengine hutibu vikundi moja, kama vile wanawake au watoto. Wengine wana husika katika sehemu ao mwili mzima, kama vile moyo, macho, au miguu.



Lazima upange kukutana na daktari wa kibinafsi. Kabla ya kuonana na daktari wa kibinafsi, kwa kawaida unahitajika ku onyesha kwamba unaweza kulipa huduma hiyo au kwamba una assurance. Ikiwa una kuwa na assurance huenda ukalazimika kulipa malipo ya pamoja au ada ndogo (k.m., \$20-\$50) wakati wa ku anza matunzo yako.

Ikiwa hauna assurance, garama yaku pata matunzo kwa daktari kipekee inaweza kuwa bei kali sana, wakati mwingine mamia ya dola kwa kila kukutana na daktari. Kwa hivi, unaweza kuangalia kliniki za afya za jamii au ya bei chini, ambazo hutowa matunzo ya bei chini kulingana na mapato yako.

Ma Hospitali ni ya wagonjwa walio na matatizo ya afya wanaomba kufanyiwa vipimo au taratibu (kwa mfano, matibabu au upasuaji, na kazalika). Kwa kawaida, daktari wako atakuelekeza kwa hospitali au kwenyewe uta pata matunzo kiisha wewe kutoka ku Urgences. Matunzo ya hospitali ni bei kali, na unaweza kuombwa ku hakikisha kwamba utaweza kulipia matunzo hiyo au kuwa na assurance kabla ya kulazwa hospitalini. Alakini, idara za dharura za hospitali haziwezi kukunyima kiingilio kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kulipa.

Kliniki ya soins d'urgences inapatikana katika eneo mbalimbali. Ni kwa ajili ya watu walio na ugonjwa au kuumiya ambalo linahitaji matunzo ya haraka na hai ombe kwenda ku urgence. Hauna lazima ya kukutana na daktari.



Hii ni mifano ya hali inayo tunzwa katika kliniki ya soins d'urgences :

- Kuumiya au kuunguzwa moto kidogo
- Busa ku masikiyo
- Kuteuka ao ku chubuka
- Maumivu ya mulibu au kikohozi
- Mwili moto, homa au mafua
- Maambukizi ku njiya ya mkojo (UTIs)

Salles d'urgences Salles d'urgences ina tajarishwa tu ajili ya matatizo ya ghafla na makubwa ya afya ambayo yanahitaji matibabu ya haraka. Kwa mfano:

- Maumivu ya kifua au ugumu wa kupumua
- Kutokwa na damu nyingi au kulumiya kutokana na ajali
- Signe ya accident vasculaire cérébral (kama vile kufa ganzi ghafla, kuchanganyikiwa, au ugumu wa kuongea)
- Ugonjwa wa homa kubwa kwa mtoto changa au mtoto.
- Réaction allergique
- Fractures au kuumi ya zaidi



Huhitaji rendez-vous kwa kwenda ku urgences, lakini wanaweza kuwa na watu wengi wa ku tunza, na huenda ukahitaji kusubiri kwa muda mrefu ikiwa tatizo lako si kubwa. Matunzo ku urgences ina kuwa bei kali sana. Ikiwa tatizo lako haiko ya kwenda ku urgence, unapashwa kutafuta ku onana na daktari ku kliniki au ku ofisi ya daktari.

Your Health Care Rights


Nchini Marekani, una haki mbili muhimu za utunzaji wa afya: Una haki ya services d'interpretations na una haki ya usiri ama confidentialité. Wajulishe wanganga wa hospitali au wa kliniki kwamba unahitaji interprete wakati wa rendez-vous yako au ukifika ku soins d'urgences. Kila kitu kinachotokea kati yako na munganga wako wa afya ni siri kufatana na sheria. Munganga wako wa afya hawezi ku sema sema ajili hali yako ya afya na familia yako, marafiki, au employeur bila ruhusa yako.

Concepts ya Marekani ajili ya Afya

Wamarekani wengi hutembelea daktari mara moja kwa mwaka juu ya bilan de santé ili ku vumbuwa matatizo ya afya kabla haiya kuwa mbaya. Wanaenda kwa daktari wa meno mara mbili kwa mwaka ili kusafishwa meno yao ili kuepuka matatizo makubwa ya meno. Waamerika wanaamini kwamba magonjwa mengi yanaweza ku epukwa kupitiya usafi, chakula kinachofaa, mazoezi, na usingizi wa kutosha.


Propreté na usafi na wa kibinafsi

Wamarekani wengi wana oka kila siku, kupiga mswaki mara mbili kwa siku, shampoo mara kwa mara, kupaka deodorant mara moja kwa siku, na kufua nguo zao mara kwa mara. Maduka huuza aina nyingi ya vitu zinazosaidia watu kuepuka kuonekana wachafu au kuwa na harufu ya jasho. Usafi wa kibinafsi unaweza kuwa muhimu sana kwa kupata na kuwekwa kazi.



Malisho bora

Malisho bora ni kula aina nyingi ya vyakula ili kuweka mwili kuwa na afya ndjema. Hii ina maana pia kupunguza vyakula vinavyoweza kusababisha matatizo ya kiafya na magonjwa makubwa iwapo vitaliwa mara kwa mara na kwa wingi. Hizi ni pamoja na vyakula vyenye sukari nyingi, chumvi, au mafuta mengi (kwa mfano, vyakula vya kukaanga, vya sukari, na soda).



Huduma ya afya ya akili

Wamarekani wanaamini kuwa afya ya akili ni muhimu kama afya ya mwili. Afya ya akili inarejelea jinsi unavyohisi, kufikiria, na tabia unapokabiliana na maisha. Pia inahusu jinsi unavyoshughulikia mafadhaiko.

Huduma bora za afya ni pamoja na matunzo kutoka kwa mtaalamu wa afya ya akili inapobidi. Ikiwa unahisi kuwa maisha ni magumu sana na huwezi kukabiliana na shughuli za kila siku, unapashwa kutafuta huduma za afya ya akili.

Sheria za Marekani zinalinda na kusaidia watu wenye ulemavu. Assurance ya afya na usaidizi wa pesa ajili ya watu wenye ulemavu zinapatikana, na wanaofika wapya marekani wanaweza kutuma maombi ya faida hizi baada ya kuwasili.

Kuhusu Settle In

Settle In ndicho chanzo chako unachokiamini cha taarifa za kuaminika, sikivu, na muhimu kuhusu Marekani. Inapatikana katika lugha nyingi, mifumo ya kidijitali ya Settle In hutoa nyenzo muhimu, mwongozo, na usaidizi wa lugha nyingi ili kuwasaidia wapya kuendesha maisha nchini Marekani.

Kuhusu Switchboard

Switchboard ni kitovu cha rasilimali cha watoa huduma kwa wakimbizi nchini Marekani na inatoa zana, fursa za kujifunza na usaidizi wa kiufundi kuhusu mada zinazohusiana na uhamishaji.

Inafadhiliwa na ORR, Switchboard inatekelezwa na IRC.

IRC ilipokea ufadhili wa kiushindani kupitia Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya États-Unis, Utawala wa Watoto na Familia, (subvention n° 90RB0053). Mradi huo unafadhiliwa kwa 100% na fedha za shirikisho.

Yaliyomo katika waraka huu ni jukumu la waandishi pekee na si lazima yawakilishe maoni rasmi ya Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu ya Marekani, Utawala wa Watoto na Familia.